





1-855-626-0002
https://orientationontario.ca

# Orientation to Ontario

## USHIRIKI KATIKA JAMII

Kuna njia nyingi za kujihusisha katika jamii yako. Baadhi ya mifano imeelezwa hapa.

### VITUO VYA BURUDANI KATIKA JAMII

Jamii nyingi za Ontario zina mahali ambapo makundi ya jamii yanaweza kukutana. Vituo vingi pia vina viwanja vya michezo ya kuteleza, mabwawa ya kuogelea, ukumbi wa mazoezi na uwanja wa michezo. Mipango ya watu wazima na watoto ni ya bure au inatolewa kwa gharama ya chini

Piga simu *211* ili kupata kituo chako cha burudani

### MAKTABA YA UMMA

Hapa kuna baadhi ya aina za mipango ambayo inaweza kupatikana kwenye maktaba ya eneo lako:

- Kiingereza kama rasilimali ya lugha ya pili.
- Wafanyakazi wa makazi wanaotoa habari.
- Vilabu vya kazi za nyumbani kwa wanafunzi na vilabu vya kusoma kwa watoto.
- Ufikiaji wa mtandao wa umma bila malipo.
- Vitabu, CD, DVD, michezo ya video, magazeti na majarida kwa Kiingereza na lugha nyinginezo.

Ili kupata kadi ya maktaba, utahitaji aina moja ya kitambulisho rasmi (pasipoti au leseni ya udereva) na uthibitisho wa anwani yako kama vile bili ya simu, umeme au kebo.

Ili kupata maktaba ya umma ya eneo lako, tembelea Wizara ya Urithi, Michezo, Utalii, Viwanda vya Utamaduni kwa findlink.at/opl

### MAENEO YA IBADA

Chini ya Mkataba wa Haki na Uhuru, Wakanada wana uhuru wa kufuata dini zao. Ingawa Ontario ni jamii ya kilimwengu, wana Ontario wengi huonyesha imani yao kwa kukusanyika katika makanisa, masinagogi, misikiti, mahekalu na sehemu zingine za ibada.

- Tembelea findlink.at/worship
- Tazama kurasa za manjano kwenye yellowpages.ca
- Muulize mshauri wa makazi.

### KUJITOLEA

Kutoa muda wako kwa shirika ni njia nzuri ya kukutana na watu wengine, kupata uzoefu wa kikazi na kujifunza kuhusu jamii yako.

- Ili kujifunza zaidi kuhusu kujitolea, tembelea Serikali ya Ontario kwa findlink.at/MCI-Active
- Ili kupata kituo cha kujitolea katika eneo lako, tembelea Kujitolea nchini Kanada kwa volunteer.ca au Ontario Volunteer Centre Network kwenye ovcn.ca
- Kutafuta nafasi za kujitolea katika sekta ya mashirika yasiyo ya faida, tembelea charityvillage.com au findlink.at/volunteer

Funded by / Financé par :

Ontario

Immigration, Refugees and Citizenship Canada

Immigration, Réfugiés et Citoyenneté Canada

# MAHUSIANO YA KIFAMILIA.

## NDOA

Unaweza kuolewa na mtu mmoja tu kwa

wakati mmoja Ontario. Ikiwa ulifunga ndoa na mtu katika nchi au mkoa mwingine, lazima upate talaka kabla ya kuoa mtu mwingine kisheria huko Ontario.

Ndoa za watu wa jinsia moja ni halali katika Ontario na kote Kanada. Ontario inatambua ndoa kutoka nchi nyingine ambapo ndoa za watu wa jinsia moja ni halali.

Ikiwa wewe na mwenzi wako mnaishi pamoja lakini hamjafunga ndoa mnaweza kuchukuliwa kuwa wapenzi wa kawaida. Wenzi chini ya sheria za kawaida lazima wawe katika uhusiano wa ndoa kwa zaidi ya miaka mitatu, au kwa mwaka mmoja ikiwa wamejaliwa mtoto.

## TALAKA

Mpenzi yeyote anaweza kuomba talaka. Ni mahakama pekee inayoweza kukupa talaka, lakini unaweza kupeana talaka bila kulazimika kwenda mahakamani kwa kutumia upatanishi, majadiliano au mazungumzo kati ya wanasheria. Wapenzi chini ya sheria ya kawaida wanaotengana wanaweza kukabiliwa na masuala ya kisheria linapokuja suala la mali na malezi ya mtoto, kwa hivyo ni muhimu kutafuta ushauri wa kisheria

## UNYANYASAJI WA NYUMBANI

Aina zote za unyanyasaji wa kimwili dhidi ya mke au mume, mpenzi chini ya sheria ya kawaida au wanafamilia wengine wowote ni kinyume cha sheria. Hii ni pamoja na matendo ya ngono yasiyokubalika. Kutishia kuumiza au kuua mtu pia ni uhalifu. Mtu yeyote atayepatikana na hatia ya unyanyasaji wa nyumbani hupewa adhabu kali, ikiwemo kifungo.

Ikiwa uko katika hatari, piga simu *911* na uitishe polisi.

Wanawake wanaopitia unyanyasaji kutoka kwa mwanafamilia au mtu mwingine yeyote wanaweza kupiga simu

Nambari ya Msaada kwa Wanawake Waliovamiwa katika

*1-866-863-0511*, masaa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki. Kwa habari zaidi, tembelea awhl.org Huduma za simu zinapatikana katika lugha 154.

## UNYANYASAJI WA WATOTO

Unyanyasaji wa watoto ni aina yoyote ya unyanyasaji wa kimwili, kihisia na/au kingono au ukosefu wa matunzo unaosababisha majeraha au madhara ya kihisia kwa mtoto au kijana. Aina za unyanyasaji wa watoto na vijana zinajumuisha unyanyasaji wa kihisia, kimwili au kingono (kutagusana au kutotagusana kimwili), kuathiriwa na unyanyasaji wa familia na kutelekezwa. Kutelekeza kunaweza kutambuliwa kwa kushindwa kutoa makazi, chakula, mavazi, elimu, usafi, usimamizi, huduma za afya, mapumziko ya kutosha, mwongozo wa kimaadili, mazoezi, mazingira salama na hewa safi

Pata maelezo zaidi kuhusu unyanyasaji wa watoto na kutelekezwa kwenye justice.gc.ca au findlink.at/protechild

Ili kupata maelezo zaidi kuhusu sheria ya familia huko Ontario, ikijumuisha haki na wajibu wako, tembelea Wizara ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika ontario.ca au findlink.at/on-famlaw

Ili kujifunza kuhusu haki za wanawake chini ya sheria ya familia ya Ontario, tembelea Elimu ya Sheria ya Familia kwa Wanawake katika onefamilylaw.ca

Ili kupata usaidizi kwa waathiriwa wa unyanyasaji wa kingono au wa nyumbani, tembelea Saraka ya Wanawake ya Ontario kwenye ontario.ca au findlink.at/serviwomen

Ili kupata habari zaidi kuhusu huduma za waathiriwa, tembelea ontario.ca au findlink.at/ovs

